# Kuelekea Viwango vya Pamoja vya Kimataifa Katika Utekelezaji wa Maendeleo ya Jamii

Mwongozo kwa Muhtasari











iACD
International Association for Community Development
Association Internationale de Développement et D'Action Communautaires

WITHOUT COMMUNITY DEVELOPMENT
THERE IS NO SUSTAINABLE DEVELOPMENT

**Baada ya kupitisha ufafanuzi wake kimataifa wa maendeleo ya jamii mnamo 2016, IACD ilianza kazi ya kutoa mwongozo wa utendakazi wa maendeleo ya jami. IACD ilifanya kazi na Jumuiya ya Kujifunza na Viwango vya Baraza la Maendeleo Scotland. Kutokana na mchakato wa kina wa mashauriano na wenzake, watendaji na wanachama kutoka kote ulimwenguni, IACD ilizindua Viwango vya Ushirikiano vya Kimataifa katika Utendakazi wa Maendeleo ya Jamii, kwenye Kongamano lililofanyika Maynooth mnamo Juni 2018.**

IACD, kama shirika la kimataifa la wataalamu, wanaamini kwamba ni muhimu kuhamasisha watendakazi,wanaolipwa na wasiolipwa, kupitisha uelewa wa pamoja wa kusudi la maendeleo ya kijamii, iliyojengwa juu ya maadili ya pamoja. IACD inakusudia kusaidia viwango vya juu vya utendakazi kwa kuzingatia maoni ya pamoja kuhusu utendakazi. Ingawa inathamini tajriba faavu, haidhamini utaaluma kama kigezo cha tajriba faavu ya utendakazi.

## Utendakazi wa Maendeleo ya Jamii

Utendakazi wa Maendeleo ya Jamii hutekelezwa na watu kwa majukumu na muktadha tofauti. Kuna wale wanao nia ya kutekeleza maadili kwa maendeleo ya jamii na kupitisha njia za kutekeleza maendeleo hayo kwa jamii. Hawa ni watu wanaotambulika kama wataalamu wa utendakazi wa maendeleo ya jamii (pamoja na wale wanaoshikilia wadhifa huo lakini taaluma zao ni tofauti); wataalamu katika kazi zingine kama vile kazi ya kijamii, elimu ya watu wazima, kazi kwa vijana, nidhamu za afya, elimu ya mazingira, maendeleo ya ndani ya uchumi, mipango ya mijini, uzalishaji upya, au usanifu; na watu wanaofanya kazi katika jamii zao wenyewe. Hawa wote tunawafahamu kama watendakazi wa maendeleo ya jamii. Pia dhana hii hutumika kwa upana kujumuisha 'watendakazi wa jamii'.

## Ufafanuzi wa IACD kuhusu Maendeleo ya Jamii

"Maendeleo ya Jamii ni taaluma inayotokana na utekelezaji wa nidhamu na kitaaluma ambao unakuza udemokrasia ya ushirikiano, maendeleo kamilifu , haki, nafasi ya kiuchumi, usawa na haki ya kijamii kupitia shirika, elimu na uwezeshaji wa watu ndani ya jumuiya zao, kutegemea eneo, utambulisho au riba, katika mazingira ya mijini na vijijini."

Fafanuzi hii inajumuisha maadili ya kuiwekea msingi, kusudi na seti za taratibu za utendaji kazi.

## A. Maadili ya Kimsingi

Ufafanuzi unaeleza maadili ambayo yanapasa kuweka msingi wa utendaji:

Uwajibikaji kihaki, mshikamano, demokrasia, usawa, haki za kimazingira na kijamii. Inaonyesha utendaji kitaaluma kama ufanya kazi kulingana na viwango vya maadili vinavyozingatiwa katika miktadha tofauti na kufanya kazi na watu pamoja na mashirika mbalimbali wakiwa na ajenda tofauti.

## B. Kusudi

Katika fafanuzi kuna taarifa kuhusu madhumuni ya maendeleo ya jamii:

'Kufanya kazi na jamii kufikia ushiriki wa kidemokrasia, maendeleo endelevu, haki, nafasi za kiuchumi, usawa na haki za kijamii'.

Taarifa hii ya kiwango cha juu ya kusudi inaweza kutumika kama njia ya kupimia mwanzo wa safari na mwisho wake.

## C. Taratibu na michakato kuu

Katika fafanuzi hiyo kuna taarifa wazi kuhusu taratibu na michakato ilishirikishwa na watendaji wa maendeleo ya kijamii: "shirika, uelimishwaji na uwezeshwaji wa watu katika jamii zao...".

## D. Washiriki

Ufafanuzi wa IACD unaashiria watu walio katika jamii zao, ziwe ni za kieneo, utambulisho au kiupendeleo . Hivi ni vikundi vya kimsingi vya watu watakao fanya kazi na watendaji wa maendeleo ya kijamii. Pia watajihusisha na mashirika ya umma, mashirika ya kibinafsi na ya kibiashara katika uungaji mkono wa maadili na kusudi la maendeleo ya kijamii.

## Mada na Maeneo Muhimu

Mada nane ambazo ni msingi katika utendaji wa maendeleo ya kijamii zimeorodheshwa hapa chini pamoja na sehemu nane kuu. Kila mojawapo ya Maeneo Muhimu yana anuwai ya taarifa kuhusu utendaji ambao hutoa mwongozo kwa watendaji wa maendeleo ya jamii. Habari zaidi inapatikana katika Makala kuu ya Viwango.

| Kichwa cha Mada | Ufafanuzi wa Mada | Maeneo Muhimu |
|---|---|---|
| **1. Maadili katika Utendaji** | Mada hii inazingatia uelewa wa maadili ambayo yanasisitiza utendaji wa maendeleo ya kijamii katika muktadha wote, michakato ya msingi wake na matokeo yanayotokana kwayo; na matumizi ya uelewa huu katika muktadha wa mtendaji mwenyewe | Kuelewa maadili, taratibu na matokeo ya maendeleo ya jamii, na kuyashikirisha katika maeneo mengine yote muhimu. |
| **2. Kushirikisha Jamii** | Mada hii inazingatia kuelewa jamii inayofanya kazi na watendaji, kuelewa maswala yanayowaathiri na kukuza uhusiano ambao huweka msingi wa utendaji kazi inayoleta mabadiliko mazuri | Kuelewa na kushirikisha jamii, kujenga na kudumisha uhusiano wa watu binafsi na vikundi |
| **3. Kuhakikisha Upangaji wa Ushiriki** | Mada hii inaangazia ukuzaji ushiriki wa jamii na uwezeshwaji wa mashirika na kusaidia jamii na mashirik kukuza ujuzi wa uendelezaji haya | Kukuza na kusaidia utendaji wa ushirikiano na ushiriki wa kijamii |
| **4. Upangaji mabadiliko** | Mada hii inaangazia uwezeshaji jamii kuchukua hatua za pamoja na kukuza stadi zinazohitajika. Pia kukuza muktadha ambapo hatua zao za pamoja zinakuzwa na kusaidiwa kama nguvu chanya ya kuleta mabadiliko. | Kuwezesha jamii kuchukua hatua ya pamoja, kuhimiza na ikiwezekena, uwezo wa kufikia, kusimamia na kudhibiti rasilimali na huduma |
| **5. Ujifunzaji kwa mabadiliko** | Mada hii inazingatia uwezeshaji ujifunzaji wa watu katika jamii na watendaji wanaofanya kazi nao katika kusaidia vipaumbele vyao katika kuleta mabadiliko na maendeleo | Kusaidia watu na mashirika kujifunza pamoja na kukuza uelewa, ujasiri na ujuzi unaohitajika kwa mabadiliko ya kijamii |
| **6. Ukuzaji Uongozi na miundombinu** | Mada hii inazingatia utambuzi Wa utofauti na kusaidia katika ujumuishaji kama jambo la msingi la utendaji. | Kubuni na kutoa mikataba, sera, miundo na mipango inayotambulisha na kuheshimu utofauti na kukuza ushirikisho |
| **7. Kuendeleza na kuboresha sera na utendaji** | Mada hii inaangazia kukuza uwezeshwaji wa uongozi katika jamii na kukuza miundombinu kwa maendeleo ya jamii na maendeleo endelevu ya mabadiliko ya kijamii. | Kuwezesha na kusaidia maendeleo ya shirika na miundombinu kwa maendeleo ya jamii,katika kukuza na kutoa uwezeshaji wa uongozi |
| **8. Kukuza Utofauti na Ushirikisho** | Mada hii inazingatia utumiaji Wa ushahidi kutoka kwa tathmini za utendaji, na kutoka kwa uchambuzi wa vipengele muhimu, ili kufahamisha na kukuza utendaji. na kukuza sera na mazoezi. | Kujenga, kutathmini na kujulisha utendaji na sera kwa maendeleo ya jamii, kwa kutumia tathmini ya utendaji kujulisha na kuboresha mkakati na mazoezi ya utendaji |

# Viwango vya kimataifa vinaweza kutumiwaje?

Viwango hivi vinaweza kutumika kama mwongozo kusaidia kwa pamoja kutambua mwisho wa safari (matokeo) na utambuzi wa safari (mchakato). Pia vinaweza kutumiwa kutafakari kwa kina Mchakato wa safari na mwisho wake. Kwa maneno mengine, Viwango vitatumika kupanga, kutekeleza na kukagua hatua na kisha kutoa msaada wa ujifunzaji kutokana na mchakato. Hivyo, vitatumiwa na watendaji wote wa maendeleo ya jamii nchini kwa njia nyingi kwa mfano :

- kujenga ufahamu wa pamoja na uelewa wa maana ya maendeleo ya kijamii
- kukuza maadili ambayo ni msingi wa maendeleo ya jamii
- kukuza utendaji
- Kuarifu nadharia na sera
- Kujenga ufunzaji na masomo ya utendaji

Tunatumai kuwa viwango hivi vitakuzwa na watendaji wa maendeleo ya jamii na kutumika kwa njia inayofaa katika nchi ambazo viwango vya kimataifa na mifumo tayari ipo, na kama rasilimali inayotoa mwongozo katika nchi ambazo viwango vya kimataifa havijaundwa.Kama sehemu ya mchakato wa mashauriano kuhusu rasimu ya Viwango , tuliuliza maoni maalum juu ya namna Viwango vinaweza kutumiwa. Tumejumuisha habari hizi hapa chini:

- Ili kuzua majadiliano juu ya madhumuni, maadili na maeneo muhimu ya maendeleo ya jamii katika mazingira ya kimataifa na ya kieneo, ndani na kati ya jamii na kati ya mashirika mbalimbali
- Kujenga rasilimali zinazosaida kuonyesha namna mazingira tofauti huathiri maeneo ya utendaji katika nchi au jamii mbalimbali
- Kujenga ushirikiano wa kimataifa na kushiriki kwa upamoja tajriba na mifano ya utendaji
- Kujenga uelewa wa pamoja katika jamii na katika mashirika kuhusu madhumuni na maadili muhimu kuhusu maendeleo ya jamii
- Kuunga mkono majadiliano juu ya upangaji shirikishi na umiliki wa kijamii ambayo hujenga hatua za pamoja na uwezeshaji
- Kuweka wazi muundo wa mafunzo ya elimu ya watendakazi wa jamii kabla na wakati wakiwa kazini.
- Kujenga tathmini ya kipekee kuhusu vifaa vya ujifunzaji
- Kusaidia kujenga taarifa kutoka ‘eneo la maendeleo’ kupeana mifano ya jinsi viwango vinatumiwa kusaidia utendaji wa maendeleo – hasa kwa kila Maeneo muhimu - mifano ya kimataifa katika mada zinazoshirikishwa.
- Kujenga rasilimali za kimataifa za kushirikishwa katika mipango ya usomi na ufundisho – kuweka wazi utendaji wa kiwango cha juu
- Kufahamisha Jamii ya ubadilishaji IACD ya Maendeleo ya Kimataifa (GCDEX) kumbukumbu za rasilimali ya ufundishaji na ujifunzaji
- Kujenga ‘msingi bora’ utakaowezesha utafiti wa kimataifa na ufadhili wa usomi ili kutalii maeneo ya utendaji wa maendeleo ya jamii.

## Kwa habari zaidi kuhusu IACD au makala yote ya Viwango vya Kimataifa vya Ushirikiano, wasiliana nasi kupitia:

**t:+44 141 248 1924 e: info@iacdglobal.org | www.iacdglobal.org**

**facebook.com/IACDglobal/ @IACD_global @IACDglobal**

**International Association for Community Development**

## Kwa maelezo zaidi namna ya kuwa mwanachama wa IACD tafhadhali enda kwa:

**www.iacdglobal.org/join-us/**

© IACD 2020

International Association for Community Development, Baltic Chambers, Suite 305, 50 Wellington Street, Glasgow G2 6HJ, Scotland, UK